



# Wauzaji,watumiaji dawa za kulevya walivyobanwa ndani ya mipaka nchini

Na REHEMA MAIGALA

SERIKALI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA),imekuwa na juhudi kubwa ya kuhakikisha uingizaji, utumiaji na usafirishaji wa dawa za kulevya nchini unapungua kwa kiasi kikubwa.

Lengo ni kuhakikisha Taifa linakuwa na vijana walio na nguvu, shupavu,hodari na wenye kufikiria maendeleo endelevu kwa nchi yao.

Hatua hiyo itazalisha vijana hodari kwa kiasi kikubwa, kupunguza utuimiaji wa dawa za kulevya kwa vijana wa kitanzania ambao baadhi yao wameathirika.

Akizungumza mwandishi wa makala hii, Kamishna wa Kinga na Tiba wa (DCEA), Peter Mfisi, anasema hivi sasa kuna udhibiti wa usafirishaji wa watu na bidhaa kwa njia ya barabara, hasa katika maeneo ya mipakani ikiwa ni hatua ya kuzuia usafirishaji wa dawa za kulevya aina ya heroin kwenda nchini Marekani.

Anasema hali hiyo imesababisha bei ya dawa hizo zinazozalisha nchini kushuka kutokana na kushindikana kuvushwa mipakani kwenda nchi za Mashariki mwa Asia.

Kamishna Mfisi anasema licha ya kuhakikisha uingizaji na usafirishaji unapungua, pia inadhibiti uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini.

Anasema katika utekelezaji wa mkakati huo mamlaka imejikita katika ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za wanaojihusisha na dawa za kulevya, ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya ,kudhibiti uzalishaji wa dawa za kulevya (kilimo na uzalishaji), kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na kuandaa na kusimamia miongozo ya utekelezaji wa dawa hizo.

Mkakati huo unalenga katika utoaji wa elimu kwa jamii, ili kuiepusha isiingie katika matumizi na biashara ya dawa za kulevya .

**DAWA ZA SHAMBANI**

Kamishna Mfisi anasema bado Tanzania inaendelea na juhudi za kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya za shambani, kama vile bangi, mirungi na zile zilizozalishwa viwandani zikiwemo cocaine na heroin.

"Kwa kudhibiti hivyo hadi sasa jumla ya tani 13.23 za bangi zimekamatwa na kuhusisha watuhumiwa 7,601, na mashamba ya bangi 28 yenye ukubwa wa ekari 26.2 yakihusisha watuhumiwa 34, yaligundulika na kuteketezwa kwa mujibu wa sheria,"anasema Kamishna Mfisi.

Anasema kwa upande wa mirungi, tani 1,180 zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa 1,156 hiyo ilitokana na kuihusisha mifumo ya kieletroniki ya 'precursors Incident Communication System (PICS) na Project Ion,"iliyosaidia kwa kiasi kikubwa kubaini na kukamata mirungi iliyokuwa inasafirishwa kwa njia ya vifurushi kutoka nchini Ethiopia kupitia Tanzania, kwenda Amerika Kaskazini.

"Kwa kuwa tumeshajiwekea udhibiti,usafirishaji na uingizaji wa dawa za kulevya hivyo kuanzia mwaka 2017 hadi 2020, takwimu zinaonyesha kiasi cha bangi kilichokamatwa kiliendelea kupungua na kiasi cha mirungi kilichokamatwa mwaka 2020 kiliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019,"anasema.

**DAWA ZENYE ASILI YA ULEVI**

Kuimarika kwa udhibiti wa dawa za kulevya kama vile heroin na cocaine kumesababisha watu kujihusisha na matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya, kama mbadala wa dawa hizo hasa katika maeneo ya mjini.

Anasema udhibiti wa dawa tiba zenye asili ya kulevya ulifanyika mwaka 2020 ambapo kampuni na maduka 77 yalikaguliwa katika mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Shinyanga Geita, Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Manyara, na Dodoma.

Hivyo, anasema ukaguzi huo ulibaini uwepo wa uhitaji mkubwa wa dawa hizo kwa matumizi haramu na dawa hizo hutolewa bila cheti cha daktari .

**NAIBU WAZIRI**

Akizungumza katika makala hii,Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu aneyeshughulikia Kazi,Vijana,na Ajira, Patrobas Katambi, anaelezea madhara ya dawa za kulevya kwa vijana na namba zinavyoathiri Taifa, akisema Serikali itaendelea kudhibiti usafirishaji na uingizaji wa dawa hizo.

Katambi anasema utumiaji wa dawa za kulevya una athari kubwa kwa vijana, kwa sababu anafanya vitu ambavyo si lengo lake na yanamsababishia kupoteza ndoto aliyojipangia tangu alivyokuwa mtoto.

Naibu Waziri Katambi anasema mtu yeyote akitumia dawa hizo unakuwa hayupo katika ufahamu wa kawaida hivyo anaweza kushawishika kujiingiza katika ugaidi , wizi na ngono zembe ambayo itamsababishia kupata maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi na magonjwa mengine yanayotokana na zinaa.

"Dawa za kulevya zina athari kubwa kwa jamii na hata taifa, hivyo wazazi na walezi tunatakiwa tuwe na malezi bora kwa watoto wetu, ili wasijitumbukize katika kundi hilo,"anasema Katambi.

Katambi anasema serikali inafanya jitihada nyingi kuhakikisha uingiaji wa dawa za kulevya unakuwa ni mgumu ndani ya nchi na wanaendelea kujenga majengo mengi, kwa lengo la kuwapa tiba wale wanaotumia dawa hizo

> "
> **Nilifanikiwa, niliishi sober house takribani miezi sita nilivyotoka pale nilijiona nimekuwa mwingine ikiwemo kuwa na akili timamu.**
>
> Nuru Ahmed.

Anasema hata Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM),imeeleza madhara makubwa yatokanayo na dawa za kulevya katika nchi hata dunia kwa ujumla.

**'SOBBER HOUSE**

Mratibu wa Kituo cha kutunza waraibu (sobber house), kilichopo Kigamboni Dar es Salaam Juma Mhina, anasema lengo la kituo chao ni kuiona Tanzania inakuwa na vijana shupavu kwa ajili ya kuleta maendeleo .

Anasema kituo chao kinahudumia kwa kufuata mpangilio wa hatua 12 wa usitiri wa pombe na mihadarati ikiwemo kumpeleka mtumiaji wa dawa za kulevya katika hospitali ya serikali au kituo cha afya kwa ajili ya kupata huduma ya Detoxification.

Mhina anasema huduma hiyo inasaidia kuondoa alosto katika mwili wa mtumiaji na maumivu katika mwili wake kwa sababu mtumiaji hawezi kuacha dawa gafla tu, ila anaacha kwa kufuata hatua zilizopo ikiwemo kupata ushauri nasaha kutoka kituoni hapo.

Mhina anasema,kituo chao kinatoa tiba ya muda wa miezi sita hadi mwaka mmoja na ndani ya kipindi hicho wanatoa elimu kuhusu athari za dawa hizo.

Pia, anasema wanatoa huduma za kidini kwa upande wa Kiislamu na Kikristu ili kuwaweka kiimani watumiaji hao.

"Licha ya kutoa huduma mbalimbali pia tunatoa huduma ya ujasirimali ili mtumiaji anapomaliza muda wake wa kukaa katika kituo hiki akienda nyumbani aweze kujiajiri mwenyewe, kwa kutengeneza sabauni, mishumaa na hata kufuma vitambaa kwa upande wa wanawake,"anasema.

Anasema ni kweli mtumiaji wa dawa za kulevya akitoka katika kituo hicho anakuwa hana hamu tena ya kutumia au kunywa pombe kupita kiasi kutokana na elimu aliyoipata.

Mhina anasema hiyo inatokana na elimu inayotolewa na wataalamu wa kituo hicho, ambao pia hutoa elimu hata kwa familia zilizoathirika.

"Mara nyingi tunavyokuwa na waraibu katika kituo tunawasiliana na familia yake kujua alikuwa anaishi vipi kabla hajaanza kutumia dawa, ili na sisi tuweze kumkumbusha yale maisha yake ya awali kwa ajili ya kurudi katika hali yake ya awali.

**ALIYEATHIRIKA**

Nuru Ahmed (40), ni Mkurugenzi wa kituo cha watu wanaotumia madawa ya kulevya kinachoitwa People with drugs Dependency Releaf Foundation (PEDDEREF), kilichopo Kigamboni Dar es Salaam, anasema kwa kipindi cha miaka 10 alikuwa mtumiaji wa dawa za kelevya lakini, aliamua kuacha baada ya kuona jamii inamtenga na hafikii malengo yake aliyojiwekea.

Anasema alitumia dawa za kulevya baada ya kushawishiwa na mume wake aliyemuoa na kupata watoto wawili.

Nuru anasema mume wake alivyomuoa hakujua kuwa anatumia madawa ya kulevya, lakini baada ya siku kadhaa alianza kuona mabadiliko ndani ya nyumba yakiwemo mume kuchoka wakati wote.

Baada ya kufanya uchunguzi wake wa kina aligundua kuwa anatumia dawa za kulevya, na hajui nini kilitokea hadi kutumia dawa hizo.

Nuru anasema hapo ndipo malengo yake yalipoondoka kwa sababu hali ilikuwa mbaya hadi ndugu walikaa kikao na kuamua kuwanyang'anya watoto wao.

Anasema baada ya kuona hali inazidi kuwa mbaya alijipeleka katika sober house ili kujitibia na kuachana kabisa na dawa za kulevya.

"Nilifanikiwa, niliishi sober house takribani miezi sita nilivyotoka pale nilijiona nimekuwa mwingine ikiwemo kuwa na akili timamu, "anasema Nuru.

Anasema licha ya kuishi sober house kwa muda mrefu pia mamlaka ya dawa za kulevya imefanya jitihada kubwa, ikiwemo kutoa elimu sahihi iliyomsaidia hadi leo hii kurudi kuwa mwanamke wa kawaida.